

**Mlango Uliofunguliwa Na Roho
Isumbukayo**
**(An Opened Door And A Troubled
Spirit)**

Na

John Kombo

**Mlango Uliofunguliwa Na Roho
Isumbukayo**
**(An Opened Door And A Troubled
Spirit)**

Na

John Kombo

November 22, 2012

Mlango Uliofunguliwa Na Roho Isumbukayo

“Basi nilipofika Troa kwa ajili ya Injili ya Yesu Kristo, nikafunguliwa mlango katika Bwana, sikuona raha nafsi ni mwangu kwa sababu sikumwona Tito ndugu yangu, bali niliagana nao nikaondoka kwenda Makedonia.” (2 Kor. 2:12-13)

Kama Paulo Misionari anakwenda kuhubiri injili akitarajia kukutana na watu wanaomujia au kutoka kwake na kuwatembelea wengine.

Makusanyiko yanaweza kutoa barua, au kuleta barua au vinginevyo kupeleka ujumbe kutoka kwa misionari na kuleta taarifa katika hali ya makusanyiko ya mahali fulani.

Hivyo kila anapofika misionari sehemu fulani inaweza kuwa katika taraja kwamba mmoja wa wafanya kazi wenzake ataungana naye pale.

Hayo ndio yalikuwa matarajio ya Paulo huko Troa. Taraja lake kila mara ilikuwa ni kuhubiri injili ya Kristo, utajiri usiofikirika unasemwa katika Waefeso 3:8. Hivyo nafasi yo yote katika mlolongo huu lazima mlango upatikane uliofunguka kwa ajili yetu kwa Bwana kuhubiri Injili ya Yesu Kristo.

Mlango wa Mkristo uliofunguliwa (Ufu. 3:7-8) na tunapaswa kuukubali ukweli huo pasipo shaka. Tatizo letu ni kwamba hatuoni mlango ukiwa umefunguliwa mara zote kwa sababu tumetingwa na mambo yasio ya kiroho.

Katika msitari wa 13, Paulo anasema *“Sikuwa na pumziko rohani mwangu. Paulo alisumbuliwa kwa sababu alitarajia kumkuta Tito alipofika lakini hakumkuta.*

Wakristo mara zote wanapaswa kumshinda Shetani; atakimbia (Yakobo 4:7). Shetani ana mbinu nyingi (Efe. 6:11) njia, mbinu, silaha n.k.

Watumishi wa Mungu, Washindi katika Kristo

Ila Mungu ashukuriwe anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu. Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo, mbele za Mungu katika wao wanaokolewa na katika wao wanaopotea,” (2 Kor. 2:14-15)

Tunapaswa, kwa umbali jinsi inavyotuhusu, kumsifu na kumpa Mungu shukrani. Paulo alimpa Mungu shukrani. Alishukuru na kumsifu Mungu kwa nafasi. Mungu alionyesha mlango uliofunguliwa kwa Paulo.

Ndugu Ellis walipofika Kenya, hasa Nakuru, tulikuwa na nafasi ya kusikia. Mungu alifungua milango kwentu kwenda. Mara zote Mungu atatufanya tuingie katika Kristo kwa kufuata na kufundisha ukweli. Majaribu, maumivu, kukata tamaa, ndio, kushindwa katika nyanja za kazi, hupaswi kumanisha kwamba kusudi la Mungu limepotea kabisa.

Katika msitari wa 15, Paulo anasema, “*Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo.*” Toka ndugu Ellis atuache tumejaribu kila mara tuwezavyo, ili kuwafikia wengine. Tunakumbana na pingamizi hasa kutoka kwa wale wanaoamini katika vikombe vingi. Wanatazama na kuongea kinyume chetu. Kulingana na wao, sisi ni waasi na hivyo tunafundisha injili nyingine (Gal. 1:6-9). Lakini wengine wanaona mwanga na kuukubali kweli.

Hataiyo, kazi ya kuifanya injili ijulikane ni kutuma manukato ya aroma mbele za Mungu. Iwe mafundisho yanafanywa kwa wale watakaotii au kwa wale watakaoendelea kuukataa. Neno lilihitimisha kazi yake kama jinsi Mungu alivyoitengeza (Isa. 55:11).

John Kombo Nandwa

Baruti Kanisa la Kristo

Nakuru, Kenya

